**HOTUBA YA CEO WA HOSPITALI YA SURVIVAL KATIKA MAADHIMISHO YA SIKUKUU YA WAFANYAKAZI DUNIANI**
**MEI MOSI -2025**

**Ndugu Wafanyakazi wa Hospitali ya Survival**

**“Assalaamu Alaikum Warahmatullahi Wabarakatuh”**

**“Bwana Asifiwe”**

**“Tumsifu Yesu Kristu”**

**“Utukufu wa Bwana”**

Leo ni siku ya pekee duniani kote tunapoadhimisha mchango mkubwa wa wafanyakazi katika ujenzi wa jamii na maendeleo ya taifa. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, nimesimama mbele yenu leo kuwatambua, kuwapongeza, na kuwashukuru kwa kazi kubwa mnayofanya kila siku kwa uaminifu, weledi na moyo wa kujitolea.

Wafanyakazi wenzangu, **jamii ndiyo wateja wetu**, na sisi ndio daraja linalowaunganisha na huduma za afya bora. Naomba niwatie moyo, muendelee kufanya kazi kwa bidii na uaminifu, mkijua kuwa kila tabasamu, kila uponyaji, na kila huduma nzuri mnayotoa inaongeza uaminifu kwa taasisi yetu. Tujenge jina la hospitali yetu kupitia kazi bora, matendo ya huruma, na kuhudumia kwa moyo wa kujali.

**Mshikamano, subira na ari ya kufanikisha malengo** yetu ni nguzo muhimu. Tuwe wamoja, tuvumiliane, tushirikiane. Hii ni familia, na mafanikio ya mmoja ni mafanikio ya wote. Tushikamane katika ndoto yetu ya kuwa hospitali bora inayoheshimika si tu Kyerwa au Karagwe, bali Kagera nzima na hata Tanzanmia kwa ujumla.

Viongozi wetu wa hospitali, serikali na jamii ni nguzo za mafanikio yetu. **Tuendelee kuwaheshimu**, kuwapa ushirikiano, na kutunza maadili mema ya kitaaluma na kibinadamu. Maadili ndiyo msingi wa taasisi yoyote inayotegemewa.

Tutumie siku hii kama fursa ya kujitathmini na kuimarisha huduma kwa mama na mtoto na idara zingine . **Mama na mtoto ndio moyo wa jamii.** Tukiboresha huduma kwao, tutakuwa tumegusa jamii nzima. Na pale ambapo kumetokea changamoto katika huduma, tuwajibike kwa moyo wa kujirekebisha bila kisingizio – kwa gharama yoyote na hali yoyote.

Binafsi natambua na kuhesimu namna mnavyojitoa kupambania ukuaji. Najua kila mmoja wenu anatamani Survival ambayo ni tumaini jema kwa jamii, wagonjwa na wafanya kazi. Tusijali! Wajibu wetu ni kuitengeneza wenyewe kwa kuwa msitari namba moja katika kutengeneza na kuheshimu dira, maono na malengo wakati kwa kuitengeneza taasisi tunayo hitaji.

## MAFANIKIO YETU.

Mambo yanayoweza kutufanya tujivunie kuwa sehemu ya Hospitali ya Survival. Hospitali yetu haina mshindani mkubwa katika sehemu ilipo kijiografia isipokuwa vituo vya afya vya serikali, jambo linalotuonyesha kuwa bado tuna nafasi ya kuwa kimbilio la wengi.

i. Tupo karibu na miji yenye watu wengi kama Nkwenda, Kayanga, Omurushaka na Morongo, hivyo tukiboresha huduma zetu tutakuwa tumewasogezea huduma wanayo stahili na hivyo kuwapunguzia adha ya kusafiri muda mrefu kufuata huduma bora.
ii. Mazingira yetu ni mazuri, na yana miundombinu safi salama na ya kuvutia ni fursa ya pekee kwa sisi kuongeza vifaa na huduma bora.
iii. Tuna mikakati madhubuti ya kuimarisha vitengo vya uzazi, mama na mtoto, upasuaji, mionzi, macho, kinywa na meno, pamoja na mortuary. Hii itatufanya kuwa Taasisi ya kipekee na ya mfano katika ukanda wetu. Hivyo tutaweza pia kuwahudumia wagonjwa wanao tokea nchi jirani kama Uganda, Rwanda, Burundi ambapo kwa sasa kijeografia tupo karibu yao. Tunapaswa tuwe baribu yao kwa huduma pia.
iv. Tuna ambulance inayotegemewa katika wilaya yetu na hata mkoani Kagera hii inatuweka katika mazingira mazuri ya kuwahisha rufaa pale inapo bidi.
v. Tunalo Duka la dawa la mfano katika ukanda wetu, duka ambalo hakuna dawa isiyoweza kupatikan.
vi. Tuna wafanyakazi wenye ujuzi wa hali ya juu, na bado tuna nafasi ya kupokea wengine kadri bajeti inavyoruhusu na pale uhitaji unapo tokea.
vii. Tuna eneo kubwa, na mipango yetu ya kuwa na Chuo cha Afya ndani ya hospitali mipango yetu inaendelea kuchukua mwelekeo mzuri.
viii. Na mengine mengi ya kujivunia kuwa sehemu ya Taasisi ya Survival

## HITIMISHO

Kwa kumalizia, nawasihi sana tumuamini na tumtegemee Mungu kwa kila jambo. Tusisahau kusali mara kwa mara, tuendelee kudumisha amani, haki, upendo, na maadili ya taasisi yetu. Tushirikiane kwa karibu na taasisi za dini, serikali, na jamii kwa ujumla. Maendeleo ya hospitali yetu yanahitaji mshikamano wa watu wote.

Wafanyakazi wenzangu, sikilizeni jamii, hudumieni kwa upendo, jiheshimuni, na mheshimu kazi yenu. Hapa tulipo si mwisho, bali ni mwanzo wa safari ya mafanikio makubwa.

Nawatakia Mei Mosi Njema.

Asanteni sana kwa kunisikiliza**.**

**CPA.RUTENGE**
**CEO**